

# SOMO LA 3

KITABU CHA MWEZESHAJI

KOZI YA “JUKUMU LA KUJIZIDISHA”

Kupanda Makanisa Yenye Afya



**Mtando wa Kuzidisha**  
Makanisa Mengi Zaidi, Makanisa Yenye Nguvu

**"JUKUMU LA KUZIDISHA"**

MAELEZO YA MTAALA WA KUPANDA KANISA | OMEGA – MNM

SOMO LA 1 PANDA KANISA LENYE AFYA	KUANDAA KUSHIRIKISHA HABARI NIEMA	SOMO LA 3 KUFAHAMU MPANGO WA MUNGU	KUSHIRIKISHA HABARI NIEMA	SOMO LA 4 MUNGU ANANIONYESHA NINI: SHIRIKISHA UTAFITI WAKO	KUWAELEKEZA WATU KUELEKEA KWENYE IMANI	SOMO LA 5 KANUNI ZA KUFUASA KWENYE MAFANIKIO
IBADA	Misingi ya Kibiblia ya Makanisa Yenye Afya	Misingi ya Kitheoloja ya Makanisa Yenye Afya	Misingi ya Kimisioloja ya Makanisa Yenye Afya	Misingi ya Kimkakati ya Makanisa Yenye Afya	Kuiishi Injili	Ukuaji wa Mkristo: Kristo Kituo Muhimu (Kristo kama Kinii)
SEHEMU YA 1	KANISA LENYE AFYA NI NINI?	RAMANI YA KIROHO: KANUNI ZA UTAFITI	HAKI KWA IMANI	VIZUIZI VYA INJILI	WITO MKUU NA KUPANDA KANISA	
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi/Usahili	Kazi, Andiko, na Muktadha	Maono, Andiko, na Muktadha	Tambuliwa Katika Wito wa Kimungu	Uinjilisti, Uanafunzi	
SEHEMU YA 2	NANI MPANDA KANISA LENYE AFYA	HIKI NDICHO YESU ALICHONIFANYA! KUELEZA NA KUSHIRIKISHA USHUUHUDA USHUUHUDA WAKO BINAFSI	MUNGU ANANIONYESHA NINI? SHIRIKISHA USHUUHUDA WAKO NA MTEMBEYO WAKO WA MAQMBI	KANUNI ZA KIBILILA ZA UONGOZI	MCHAKATO WA KUBADILKA I	KANUNI ZA KUFUASA KWENYE MAFANIKIO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Tambuliwa Katika Wito wa Kimungu	Uinjilisti	Kazi, Andiko, na Muktadha	Kuwaimarisha / kuwawezesha viongozi	Uinjilisti	Uanafunzi
SEHEMU YA 3	KUFIKIRI – Z: MUNGU ANATAKA NINI?	KUONGOZA VIKUNDI VIDOGO	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: KUTAMBUA MAONO YA MUNGU	UINJILISTI NA KUPANDA KANISA	MCHAKATO WA KUBADILKA II	TAMBUA LENGO LAKO, TAMBUA WATU WAKO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Uinjilisti, Uanafunzi, Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Uinjilisti	Uinjilisti	Uanafunzi
SEHEMU YA 4	MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA	NJIA YA II YA KUIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KUANGALIA NENO LA MUNGU	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA KAZI	KUANZISHA KIKUNDI KIDOGO	UINJILISTI WA KIKUNDI KIDOGO	NJIA YA IV YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KULTITUMIA NENO LA MUNGU
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Uinjilisti, Uanafunzi	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Uinjilisti, Uanafunzi	Uinjilisti	Uinjilisti, Uanafunzi
SEHEMU YA 5	KWA NINI VIKUNDI VIDOGO?	NAMNA YA KUTENGENEZA MAOMBI KATIKA UPANDAJI WAKO WA KANISA	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA MSINGI	UINJILISTI NA KUFIKIA MAHTAJI YA JAMII	UTENDAJI: UZOFFU WA KIKUNDI KIDOGO	KUELEWA MTAZAMO WA KIDUNIA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uinjilisti, Uanafunzi	Uinjilisti	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Huduma	Uinjilisti	Tambuliwa Katika Wito wa Kimungu
SEHEMU YA 6	NJIA YA I YA KUIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: HEBU BIBLIA ITUFUNDISHE	TAMASHA LA MAOMBII: ZABURI 95	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA MKAKATI	KUWASILISHA MIPANGO MIKUU NENO LA MUNGU		TAMASHA LA MAOMBI LA KUMSHUKURU MUNGU KWA JAMINIFU WAKE
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uinjilisti, Uanafunzi	Kuabudu	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Uinjilisti, Uanafunzi	Mchanganyiko wa Mawazo	Kuabudu

<b>SOMO LA 7 TENGENEZA TIMU</b>	<b>SOMO LA 8 TENGENEZA TIMU</b>	<b>SOMO LA 9 KUWAJALI WATU</b>	<b>SOMO LA 10 KUANZISHA KANSIA</b>	<b>SOMO LA 11 KUPANGA KWA AULI YA MAMBO YAJAYO</b>	<b>SOMO LA 12 KUENDELEA MBELE KWA UMOJA</b>
IBADA	Kubadilishwa na Injili	Neema ni kwa wanyenyekewu	Upendo, Msingi wa Huduma	Iii Ulimwengu Upate Kuamini: Yohana 17	Kuhesabu Gharama
<b>SEHEMU YA 1</b>	<b>MISINGI YA KIBILIA YA KANISA</b>	<b>KAZI YA TIMU: KUFANYA KAZI NA WENGINE KWA USAHIIHI</b>	<b>UINJILISTI WA KIMAHUSIANO</b>	<b>KAZI ZA USHIRIKA ZA KANISA</b>	<b>UTANGULIZI KATIKA UWAKILI</b>
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganiko wa Mawazo	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwajali washirika wa kikundi kidogo	Mchanganiko wa Mawazo	Uwakili wa Rasilimali
<b>SEHEMU YA 2</b>	<b>KANISA: KIUMBÉ HAI</b>	<b>KUANZISHA TIMU</b>	<b>USHIRIKA</b>	<b>HUDUMA KUPITIA KARAMA ZA KIROHO</b>	<b>TOBA KAMA NAMNA YA MAISHA</b>
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganiko wa Mawazo	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Ushirika	Kuanganisha Mwili Kutohana na Karama za Kiroho	Uwakili wa Rasilimali
<b>SEHEMU YA 3</b>	<b>KIKUNDI CHA WATU KINAKUWA KANISA LINI?</b>	<b>UHAI KATIKA MIADALA WA KIKUNDI KIDOGO</b>	<b>KUJUAL JAMII YETU</b>	<b>NAMNA YA KUTUMIA TATHMINI YA KARAMA ZA KIROHO</b>	<b>TOBA NA UREJESHO: NIDHAMU YA KANISA</b>
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganiko wa Mawazo	Uanafunzi	Uinjili, Andiko, na Muktadha	Kuanganisha Mwili kutohana na Karama za Kiroho	Ushirika
<b>SEHEMU YA 4</b>	<b>NUJA YA V YA KUIFUNZA BIBLIA KWА NJIA ELEKEZI; NUJA ZA KUTUMIA MAFUNZO ELEKEZI YA KUIFUNZA BIBLIA</b>	<b>KUWAJUNDISHA VIONGOZI WAPYA WA VIKUNDI VIDOGO</b>	<b>TABIA ZA KANISA LINALOKUWA</b>	<b>UHAI WA VITA YA V KIROHO</b>	<b>MITINDO YA UONGOZI</b>
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uanafunzi	Uanafunzi, Kuimarisaha/ Kuwawezesha viongozi	Mchanganiko wa Mawazo	Ushirika	<b>SEMINA YA MPANGO MKAKATI I</b>
<b>SEHEMU YA 5</b>	<b>MWONEKANO WA KIONGOZI MKRISTO</b>	<b>MITINDO YA KUIJICHANGANYA</b>	<b>UONGOZI WA KITUMISHI</b>	<b>NAMNA YA KULIONGOZA KANISA KATIKA KUABUDU</b>	<b>Kuwawezesha / Kuwaimarisha Vlongozzi KANISA LETU NA UKUBWA WA MWILI WA KRISTO</b>
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuabudu	Ushirika
<b>SEHEMU YA 6</b>	<b>MAHUBIRI YA KIBILIA II: KULIELEWA KUNDI / KUSANYIKO</b>	<b>MAHUBIRI YA KIBILIA III: KULIELEWA KUNDI / KUSANYIKO</b>	<b>TAMASHA LA MAOMBI: WAFFESO 3 – 5</b>	<b>MAHUBIRI YA KIBILIA III: KUJIELEWA WEWE MWENYEWEE</b>	<b>TAMASHA LA MAOMBI: KUOMBEA KUENEZA INJILI</b>
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuabudu	Kuabudu	Ushirika	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahili	Unjiliisti

**JUKUMU LA KUJIZIDISHA**  
**Masomo ya Kupanda Makanisa Yenye Afya**  
**Huduma ya Mtandao wa Kujizidisha**  
**Makanisa Zaidi/Makanisa yenye Nguvu**  
Hakimiliki© 2015



Masomo haya ya mafunzo ya upandaji kanisa ni mjumuisho wa kozi ya Abridged Omega na mafunzo ya Kupanda Makanisa Yenye Afya ya Mtandao wa Huduma ya Kujizidisha.

MNM imepata ruhusa ya kuweka wazi kazi hii itumiwe na kanisa kutoka katika Kituo cha Mafunzo ya Upandaji wa Makanisa na Huduma za Ulimwengu.

**Unaruhusiwa na kutiwa moyo kuzalisha na kusambaza masomo haya** kwa muundo wa aina yoyote yatakavyotolewa kwamba: (1) utambue / ushukuru chanzo (2) onyesha ikiwa marekebesho yamefanyika, (3) usitoze gharama zaidi ya ile ya kuzalisha, na (4) usizalishe nakala zaidi ya 1,000.

Kozi ya OMEGA:

Mafunzo ya Vitendo ya Kupanda Kanisa

Hakimiliki © 2000, 2006 United World Mission.

Masomo haya mwanzoni yalimiliwi na Alliance for Saturation Church Planting na kuandaliwa na huo ubia kwa kushirikiana na Huduma ya Peter Deyneka Russian, Mradi 250.

Kama ungependa kuyarusha masomo haya kwenye mtandao au kama umedhamiria kutumia zaidi ya ilivyotajwa hapo juu, tafadhali wasiliana na United World Mission, ATTN: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pine Blvd., Charlotte, NC 28273-5596, au omega\_course@alliancescp.org.

Tafsiri na matoleo katika mazingira yako pia yanaruhusiwa.

Tunamshukuru Dr. Jerry Wofford na Dr. Jeff Hale kwa mchango wao usioweza kulipwa katika kuandaa masomo haya. Gary Teja na John Wagenveld, wahariri wa Kazi ya Kujizidisha

**[www.multiplicationnetwork.org](http://www.multiplicationnetwork.org)**

<b>PENDEKEZO LA MUUNDO WA SIKU 1 WA MAFUNZO YA SOMO LA 3</b>		
	UTANGULIZI WA SOMO LA 3	2:00
	IBADA	2:15
	KUTOA TAARIFA	2:30
KIPINDI CHA KWANZA	MUNGU ANANIONYESHA NINI: SHIRIKISHA UTAFITI WAKO	3:00
	MAPUMZIKO	4:00
KIPINDI CHA PILI	MUNGU ANANIONYESHA NINI: SHIRIKISHA USHUHUDA WAKO NA UZOEFU WAKO WA KUTEMBEA KATIKA MAOMBI	4:15
KIPINDI CHA TATU	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAONO	5:15
	CHAKULA CHA MCHANNA	6:15
KIPINDI CHA NNE	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: DHIMA/ KAZI	7:15
KIPINDI CHA TANO	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAADILI	8:15
	MAPUMZIKO	9:15
KIPINDI CHA SITA	MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MKAKATI	9:30
	KUFUNGA	10:30
	MWISHO WA SIKU	10:45

## **FAHAMU MAONO YA MUNGU**

### **SOMO LA 3**

#### **Lengo la Kujifunza:**

- Washiriki wataweza kuelezea kwa maneno yao wenyewe kazi na tofauti kati ya
  - (a) kauli ya maono (b) kauli ya dhima (c) kauli ya maadili ya msingi, na (d) mkakati wa kupanda kanisa
- Washiriki wataanza kuendeleza kauli ya maono, kauli ya dhima, kauli ya maadili ya msingi, na mkakati wa kupanda kanisa kulingana na kuanza kwa kanisa jipya.
- Kwa kutumia Mpango wa Vitendo Somo la 4, washiriki watarudia maono yao, dhima, maadili ya msingi, na mkakati na wachungaji wao, wakisaidiana na uongozi wa kanisa, na wengine watakaojumuishwa katika upandaji wa kanisa (kwa usahihi).

**Angalizo kwa Mwezeshaji:** Ingawa “Sehemu ya 5: Mpango Wangu Mkuu wa Kupanda Kanisa: Maadili” yamepangiwa saa nzima kwenye ratiba ya somo, inaweza kuhitaji dakika kama 30 hivi. Ukubwa wa kazi utamalizika kwenye Mpango Kazi wa Mpanda Kanisa Somo la 4. Unaweza kutumia muda mwingine wa ziada kwa kadiri ya uhitaji, kwa mfano, kurudia masomo yaliyopita, kufundisha, maombi katika kikundi vidogo, kutoa maswali na changamoto walizonazo washiriki, au kuwaruhusu mapema.

#### **Utangulizi wa Somo la 3 (dakika 15)**

#### **Neno la Muwezeshaji la Utangulizi (dakika 2)**

- Kuwakaribisha washiriki kwa namna ya kirafiki, kiukarimu na kwa kufurahi.
- Waongoze washiriki kwa maombi mafupi ya pamoja, iweke siku wakfu kwa utukufu wa Mungu

#### **Shughuli ya kuanzia: Utangulizi (dakika 5)**

Kila mtu kwenye kundi ameambiwa ana dakika mbili za kufikiria swalii na kuliuliza kwa watu wengine kwenye kundi. Kwa kadiri swalii litakavyokuwa bora, ndivyo ubunifu na mwitikio utakavyoongezeka na utaupokea. Baada ya kila mmoja kufikiria swalii, wakaribishe wasimame na waambie wawaalize swalii watu wengi kwa kadiri watakavyoweza kwa dakika mbili. Andika majina ya kila mtu na jibu lake. Baada ya dakika mbili, liambie kundi likae chini na uwakaribishe watu waje kushirikisha baadhi ya vitu walivyojifunza kumhusu kila mmoja.

#### **Utangulizi wa Maono, Dhima, Maadili, na Mkakati (dakika 8)**

- Andika ubaoni maneno haya au kwenye kipande cha karatasi kilichobandikwa ukutani: Maono, Dhima, Maadili, na Mkakati.
- Uliza kundi maswali haya:
  - 1) Ni kwa namna gani ungeelezea maana ya dhana hizi?
  - 2) Ni kwa namna gani zinatofautiana?
  - 3) Maono, Kazi, Maadili, na Mkakati vinafanya nini katika kupanda kanisa?
- Sema, "Leo tunaenda kuangalia kwa pamoja umuhimu wa maono, dhima, maadili, na mkakati wa kupanda kanisa. Mitazamo hii ni njia za vitendo kwa kanisa kuelezea lenyewe ni nani na kwa nini linafanya kile linachofanya. Kwa kifupi, mitazamo hii inaelezea asili ya kanisa na kazi zake. Tunapopanda kanisa, tunatumia kanuni ya kimisiolojia (inayohusiana na umisheni), kwa hiyo tunaenda kuanza kuangalia maono, dhima, maadili, na mkakati kwa ibada fupi iliyo kwenye misingi ya kimisiolojia ya kupanda makanisa yenye afya."

## **IBADA**

### **MISINGI YA KIMISIOLOJIA KWA MAKANISA YENYE AFYA (DAKIKA 15)**

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Waambie wajitolee kusoma kwa sauti vifungu vyta Biblia kwa kila msingi wa theolojia kwa kazi ya kanisa. Ongoza kundi kugundua kila kanuni ya kimisiolojia kutoka katika vifungu viliviyosomwa na kujaza sehemu zilizo wazi za kufanana kwenye madaftari yao ya kazi.

#### **Shughuli ya kuanzia (dakika 2)**

Waambie washiriki washirikishe mawazo yao kwenye sababu za kupanda makanisa mapya. Waambie wasikilize waone ni kipi kati ya haya yaliyotajwa kwenye sehemu hii.

#### **Ibada ya Kujifunza Biblia (dakika 13).**

**KANUNI YA 1** | Vile Kanisa ni LILIVYO (kiini/asili yake).

**Soma: 1Petro 3:9-12; Waefeso 4:24; 1Wakorintho 12:12-13**

**Waulize** washiriki ni nini tumejifunza kuhusu kanisa/Watu wa Mungu katika vifungu hivi.

**Sema,** "Kanisa, jamii iliyoumbwa na Mungu kuwa watu wake, pia ni wakala wa kuibadili upya jamii na uumbaji. Kanisa ni mtu mpya aliyeumbwa ndani ya Yesu Kristo, kuwa kama Mungu katika haki ya kweli na utakatifu. Kanisa ni mwili wa Kristo, ulioungana na Roho wake kuwa familia moja."

Kanisa ni jamii mpya iliyoumbwa ndani ya Kristo Yesu, kuwa kama Mungu katika haki ya kweli na utakatifu. Kanisa ni mwili wa Kristo, uliounganishwa na Roho wake katika familia moja.

**KANUNI YA 2** | Vile Kanisa LINAVYOFANYA (kazi/kusudi lake).

**Soma:** Matendo 6:1-7, Matendo 11: 19-26 na 12:25

**Uliza:** Kanisa linafanya nini katika mistari hii?

**Sema**, "Kile ambacho kanisa linafanya kiko kwenye msingi wa kanisa ni nini. Kanisa linatangaza ufalme wa Mungu katika Yesu Kristo; linawasilisha Injili katika mazingira fulani; na kushiriki katika kazi/ misheni ya Mungu. Hapa tunaona kwamba kujengwa kwa Mkristo kunaenda bega kwa bega na kazi yake ya kutangaza, kutumika na kuhudumia. Vifungu hivi vinatukumbusha kwamba kanisa ni watu wa Mungu walio kazini. Kanisa HUFANYA kulingana na lenyewe LILIVYO. Kama mbwa anavyobweka sababu ni mbwa, kanisa linafanya dhima/ misheni kwa sababu ni kanisa."

Kile ambacho kanisa linafanya kiko kwenye msingi wa kanisa ni nani/vile lilivyo

### **KANUNI YA 3 | Kanisa LINAPANGA kile LINACHOFANYA (muundo wake/taasisi).**

**Soma** Matendo 6:1-4.

**Uliza** namna ambavyo wanafunzi waliamua kupanga kazi

**Sema**, "Mwisho, linajisimamia na kujipanga lenyewe kulingana na mazingira na mpango kazi wake ili kutekeleza kusudi lake. Kanisa linatoa muundo katika kazi zake ili kukamilisha kazi lililopewa na kufanya. Likiongozwa na Roho Mtakatifu, kanisa hupanga, hutendea kazi, hutathmini na kubadilika kulingana na dhima yake. Kanuni muhimu hapa ni kwamba ikiwa kanisa litaelewa asili na kusudi lake, litapangilia taasisi yake ili kukamilisha dhima yake."

Kanisa linapanga na kujiunda lenyewe kulingana na mazingira yake na mkakati wake wa kazi ili kutimiza kusudi lake.

### **KUTOA TAARIFA: (DAKIKA 30)**

#### **Maelekezo:**

- Kwa kutumia fomu ya taarifa ifuatayo, waongoze washiriki kushirikisha shughuli zao za kupanda makanisa toka walipokamilisha Somo la 2.
- Sherehekeea ushindi; watie moyo wale ambao inawezekana wamekata tamaa. Kadiri muda utakavyoruhusu, mnaweza kuhitaji kucombeana kila mmoja kwenye vikundi vidogo kulingana na uzoefu huu wa kupanda makanisa.
- Jibu swal lolote kuhusu mchakato wa taarifa

## ABC ZA MPANDA KANISA

TAARIFA YA MWEZI

TAARIFA ZA KAWAIDA

MWEZI WA TAARIFA		USIMAMIZI WA MAHUDHURIO YA VIKAO	NDIYO	HAPANA
JINA LA MPANDAJI				
KANDA YA MPANDAJI				
MRATIBU WA KANDA				

## BINAFSI

<b>WATU WAPYA WALIOFIKIWA</b> WATU WALIOFIKIWA KWENYE MAZINGIRA YA KUPANDA MAKANISA KULETA INJILI	
<b>WAONGOFU WAPYA</b> WAFUASI WA YESU	
<b>WATU WAPYA WALIOBATIZWA</b> WATU WALIOSHIRIKI KWENYE SAKRAMENTI YA UBATIZO	
<b>VIONGOZI WAPYA KATIKA MAFUNZO</b> WATU WANAOFUNDISHWA UONGOZI NA WAPANDAJI	

**VIKUNDI VIDOGO** | Kiwango cha chini wafuasi 2 wapya na kiongozi mmoja

<b>VIKUNDI VIDOGO VIPYA</b> VIKUNDI VILIVYOANZISHWA MWEZI HUU	
<b>WASHIRIKI WAPYA KATIKA VIKUNDI VIDOGO</b> WATU WAPYA WALIOSHIRIKI KATIKA VIKUNDI VIDOGO MWEZI HUU	
<b>VIONGOZI WAPYA NA KIKUNDI</b> VIONGOZI WAPYA NA KIKUNDI CHINI YA USIMAMIZI WA MPANDAJI	

## MAOMBI UNAYOHITAJI

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_

## SHUHUDA

---



---



---



---



---

# **KIPINDI CHA 1**

## **MUNGU ANANIONYESHA NINI: KUSHIRIKISHA UTAFITI WAKO (dakika 60)**

**Sema,** “Katika Somo la 1, uliambiwa ukamilishe Mpango Kazi wa Somo la 4: Mpango ‘Z’ wako. Katika Somo la 2 uliambiwa uchunguze maeneo ambayo una mpango wa kupanda kanisa. Maswali haya matatu katika kipengele hiki yanakupatia mchakato wa kuanza kufanya utafiti wa awali. Kabla hatujaenda kwa undani kwenye somo la utafiti, hebu tuwe na muda wa kutoa taarifa ya kile mllichopata katika kazi hii”.

### **Maelekezo ya Mwezeshaji:**

- Mpe kila mtu dakika 15 za kushirikisha matokeo ya kazi yake kwa kutumia muundo wa Mpango Kazi wa Somo la 3 kutoka katika Somo la 2 ukiwagawa katika makundi ya watu watatu. Muundo umetolewa chini kwa ajili ya msaada zaidi.
- Zungukia kila kundi kuangalia shughuli zao.
- Kama kuna watu ambao hawakumaliza kazi, panga kuzungumza nao binafsi wakati wa mapumziko. Waambie wafanye mpango wa kukamilisha kazi yao kabla ya kipindi kijacho cha mafunzo.
- Tumia dakika 15 za mwisho za kipindi kufanya muhtasari wa kazi na kundi zima.
- Muonekano wa Muundo: taarifa ya kila mtu lazima iwe kwa makadirio ya dakika 10-15 na iwe na taarifa zifuatazo:

### **1. Sehemu ya Kwanza – Taarifa za awali zilizokusanywa (dakika 5-6)**

Elezee maeneo uliyokusudia

- Ulikusanyaje taarifa zako (kutembelea, kufanya usaili usio rasmi, kufanya uchunguzi/ramani, utafiti wa maktaba, n.k.)?
- Jadili tatizo lolote kubwa au magumu wanayokutana nayo na namna wanavyoyatatua. Ungefanya nini cha tofauti wakati ujao?

### **2. Sehemu ya Pili – Kuchunguza Taarifa (dakika 5-8)**

Anayekumbusha utoaji wa taarifa lazima azingatie matokeo ya tafiti zenu. Utoaji wa taarifa lazima ujibu maswali muhimu yafuatayo:

- Ni taarifa ipi iliyokuvutia zaidi ulipofahamu kuhusu eneo ulilokusudia na watu wanaoishi hapo?
- Je kuna taarifa yoyote iliyokushangaza?
- Ni kitu gani haswa ulichojifunza kitakachokusaidia kutengeneza mpango wako wa kupanda kanisa katika eneo ulilokusudia.
- Ni jambo gani moja la muhimu ambalo kwa kupanda kanisa ulithibitisha kwamba ulikwisha fahamu ni eneo la mavuno?
- Ni kitu gani kipyta cha muhimu umekigundua ulipopanda kanisa eneo la mavuno ambacho hukukifahamu kabla?
- Ni fursa gani za mlango ulio wazi wa Injili umezipata?
- Ni vikwazo gani umekutana navyo na ni namna gani utavivuka?
- Ni utafiti gani wa ndani zaidi unaohitaji kuufanya ili kuendeleza uinjilisti shirikishi na mpango wa kupanda kanisa katika eneo ulilokusudia.

## **KIPINDI CHA 2**

### **MUNGU ANANIONYESHA NINI: SHIRIKISHA USHUHUDA WAKO NA UZOEFU WA KUTEMBEA KATIKA MAOMBI (Dakika 60).**

**Maelekezo ya Muwezeshaji:** hii ni taarifa ya shuhuda na mpango kazi wa maombi yatakayoenda katika Somo la 3 kutoka katika Somo la 2.

- Wagawe washiriki katika makundi ya watu watatu watatu.
- Waambie kila mmoja ashirikishe ushuhuda wake binafsi ule uliorudiwa na kushirikishwa hadharani toka kipindi kilichopita.
- Kwenye hayo makundi madogo, waambie kila mmoja ashirikishe mtu uzoefu wao wa kusimulia watu ushuhuda wao binafsi na maombi ya kutembea katika maeneo waliyokusudia.
- Zungukia kila kundi kuangalia mjadala wao.
- Kama kuna watu ambao hawakumaliza kazi, panga kuzungumza nao binafsi wakati wa mapumziko. Waambie wapange kumaliza kazi kabla ya kipindi cha mafunzo kinachofuata.
- Tumia dakika 15 za mwisho wa kipindi kufupisha kazi kwenye kundi kubwa (lote).

## KIPINDI CHA 3

# MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAONI (Dakika 60)

### NAMNA YA KUTENGENEZA KAULI YA MAONO

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Tumia masomo yaliyo hapo chini kutoa utangulizi wa wazo la kauli ya maono. Ongiza kundi kukamilisha shughuli zinazofuata.

Kauli ya maono ni maelezo rahisi na ya kueleweka ya namna unavyoamini Mungu anataka kundi lako liwe. Ni lazima iseme sura nzima kwa ujumla ya kundi lako katika hali kamilifu lakini ijikite vya kutosha kuwalenga watu katika utendaji halisi. Pia, lazima ielezee hali unayotenda kazi ili kuifikia, sio ile ambayo imeshakamilika.

Ili uweze kuendana na eneo lako ulilokusudia, Kauli yako ya Maono inatakiwa iakisi kile ulichojifunza kwenye utafiti wako.

### MIFANO MINNE YA KAULI YA MAONO (DAKICA 15)

- I. “Tutakuwa kanisa lililojaa Roho Mtakatifu, linalokua likimfanania Kristo.”
- II. “Tutakuwa nuru ya Kristo kwenye giza la jamii yetu.”
- III. “Tutakuwa jamii ya imani ing'aayo kwa haki na tumaini la Kristo katika kusanyiko letu, jiji, na sehemu nyingine za ulimwengu.”
- IV. “Tutakuwa kusanyiko la haki na imani, tukitumikia waliopotea vivyo hivyo na waamini wenzetu katika jamii yetu, dini, na ulimwenguni kote.”

Tambua kwamba kila kauli ya maono inaakisi kile ambacho Mungu ametufundisha katika Neno lake kuhusu Kanisa lake linatakiwa liweje. Pamoja na hivyo, kauli hazifanani katika utendaji kama kauli za maono.

- I. KAULI YA KWANZA inaelezeka kama neno ambalo lingeweza kuwa kweli kwa kiasi kwa sasa, na mwendelezo unaotarajiwu kwa muda wa ziada. Haina upekee maalum wa kazi za kundi au huduma katika mwelekeo wa nini cha kufanya.
- II. KAULI YA PILI haina mfumo ama umbo na inaweza kuwa ya kweli muda wowote kwa njia tofauti. Tena, haitaji tabia za kundi wala kiwango cha utendaji kihuduma.

III. KAULI YA TATU kwa kiasi fulani imekamilika, kama inavyoelezea tabia za kundi (haki na tumaini katika Kristo) na wapi watakapohudumu (kusanyiko, jiji, na sehemu nyingine za ulimwengu). Tabia na kufikiwa kwa huduma, vyote ni misingi ya mwelekeo wa nini cha kufanya.

IV. KAULI YA NNE imekamilika zaidi. Inazungumza tabia za kusanyiko, wapokeaji wa huduma wanaokusudiwa, na kufikika kimwili kwa huduma. Kanuni hizi zinaelezeka wazi na yaliyomo ni ya Kibiblia.

### **SHUGHULI (DAKIKA 45)**

1. Katika vikundi vidogo vidogo au watu wawili wawili, orodhesha maneno kadhaa yanayoliezea kusanyiko lako jipya kama vile lilikuwa sawa kulingana na kanuni za kibiblia – namna unavyoamini Mungu anataka liwe! Baadhi ya maneno yanatakiwa yawe: haki, uaminifu, upendo, furaha, huruma, ukarimu, n.k. haya maneno yanaelezea tabia za kusanyiko. Orodhesha maneno haya yanayoelezeka kwa kutumia kila neno kukamilisha sentensi:

Mungu anataka tuwe ...

---



---

2. Kisha, orodhesha unaamini utamhudumia nani kwa kukamilisha sentensi hii

Mungu anataka tumhudumie... ( nani?)

---



---

3. Mwisho, orodhesha kazi ambazo kusanyiko lako jipya litakuwa likifanya wakati likiwa katika hali nzuri. Hizi zinaweza kuwa kauli mbiu. Baadhi ya mifano ni:

- Peleka Injili ulimwenguni
- Hudumia rika zote katika jamii yetu
- Washirika wote kujihusisha na uanafunzi wa kiroho
- Nguvu ya kiuchumi kukua siku zote
- 

Unaweza kuorodhesha kazi hizi kwa kukamilisha sentensi hii:

4. Tutaelezea viwango vyetu kupitia...

---

---

---

5. Sasa, jadili na mwenzako au kikundi kidogo maneno uliyochagua kuelezea tabia halisi za kusanyiko, watu ambao kanisa litawahudumia, na kauli mbiu zionyeshe kanuni za vitendo za kusanyiko lako. Chagua tatu muhimu zaidi kwa kila orodha na uziandike.

---

---

---

6. Mwisho, andika kauli ya maono ambayo hutumia maneno muhimu yanayoelezeka, wapokeaji wa huduma, na kauli mbiu ya kazi (unaweza kutumia mfano wa tatu au wa nne wa kauli ya maono kama somo.)

---

---

---

Shirikisha kundi kubwa kauli ya maono uliyoandika. Shirikiana na kundi kubwa kuhakikisha kwamba maneno yako yanaeleweka na yanazungumzia mawazo yako kwa usahihi.

7. Angalia maneno yaliyoshirikishwa, na andika kauli ya maono ya mwisho hapa.

---

---

---

8. Ni vifungu gani kwenye biblia vinavyobeba haya maono?

---

---

---

9. Rekebisha kauli ya maono ili iwe rahisi na ya kueleweka. Ni kwa namna gani

utazungumzia haya maono kwenye timu ya kuzindua na kuwakaribisha kuyaasili/kuyamiliki maono kuwa yao? Kusanyiko litahitaji nini kuelewa na kuamini ili liweze kuendelea na maono haya? Utalisaidiaje kusanyiko kufanya hivi?

---

---

---

---

---

---

Chakula cha mchana (dakika 60)

## **KIPINDI CHA 4**

# **MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: DHIMA (Dakika 60)**

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Tumia masomo yaliyoko hapo chini kutoa utangulizi wa wazo la Kauli ya dhima. Ongoza kundi kukamilisha shughuli inayofuata.

### **NAMNA YA KUTENGENEZA KAULI YA DHIMA**

Rudia kuangalia & Wazo Jipy (dakika 15)

#### **Marejeo**

KAULI YA MAONO ni maelezo mafupi na yakuelewaka kuhusu kile unachoamini kuwa Mungu anataka kusanyiko lako liwe. MAONO yanahusu KUSANYIKO litakuwa NI NANI

#### **Dhana Mpya**

KAULI YA DHIMA ni muhtasari wa NAMNA kanisa LITAKAVYO YAFANYA MAONO KUWA HALISI.

KAULI YA DHIMA inazungumzia vitendo ambavyo vitasababisha maoni yatokee.

#### **KAULI YA DHIMA INAHUSU VITENDO.**

Ili uweze kuendana na eneo lako ulilokusudia, Kauli yako ya Dhima lazima iakisi kile ulichojifunza katika utafiti wako.

- I. Dhima ya Kanisa la Living Water ni kuiishi Injili ya Yesu Kristo kupitia kuabudu Utatu Mtakatifu wa Mungu, kuhubiri Neno, kuwashudumia majirani zetu, kufuusa waamini kuanzia watoto hadi wakubwa, na ushirika wa familia ya Mungu.
  
- II. Katika Kanisa la New Life Community tutakuwa nuru ya Kristo kupitia:
  - Kumwabudu Mungu wa kweli katika Roho na Kweli (Yohana 4:24)
  - Kuhubiri Neno la Mungu kwa namna ya kueleweka ndani na nje ya kanisa. (Mathayo 28:18-20)
  - Kuhudumia majirani na familia zetu, waliowekewa mipaka, na waliosahaulika katika jamii yetu kwa upendo wa Kristo (Marko 12:31)
  - Kukua katika imani na kusaidia wengine kukua (2Petro 3:18)

- Kuwahudumia ndugu zetu wa kiume na wa kike kwa upendo wa Kristo (Warumi 12:10,13)

### **SHUGHULI (DAKIKA 45)**

1. Makusanyiko haya yanaenda kufanya nini, kulingana na mifano ya kauli za dhima zilizo hapo juu?

---

---

---

2. Nakili kauli ya maono ya kusanyiko lako hapo chini (ulichoandika kwenye sehemu ya kazi ya 1)

---

---

---

3. Kanisa lako linataka kumfikia nani?

---

---

---

4. Ni namna gani kusanyiko lako litafikia maono yake kwa kuwafikia hawa watu? Utafanya nini kutekeleza? Orodhesha kazi halisi:

---

---

---

Tunapendekeza kwamba kila kauli ya dhima zihusishe kazi tano muhimu za kanisa:

- Mahubiri na Uinjilisti
- Elimu na uanafunzi
- Huduma
- Ushirika
- Kuabudu

5. Kauli ya dhima lazima iseme namna maono yatakavyofikiwa. Hakikisha unahusisha namna ambavyo vitendo katika kauli ya dhima vitasababisha maono yatokee (kwa nguvu za Mungu!). Rekebisha kauli yako ya dhima na uiandike hapa.

---

---

---

---

6. Ni andiko gani la Biblia linalobeba shughuli zilizoorodheshwa katika kauli yako ya dhima?

---

---

---

---

7. Shirikisha kauli yako ya maono na kauli yako ya dhima (ikiwepo msingi wake wa biblia) kwenye kundi kubwa na uziandike hapa.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

#### **MPANGO KAZI WA SOMO LA 4**

Shirikisha maono yako na kazi yako kwa mchungaji na kanisa linalokusaidia.

Kabla ya kurudi kwenye somo la 4, shirikisha kauli ya maono na kauli yako ya dhima (ni pamoja na misingi yake kwenye biblia) pamoja na timu ya kuzindua, kanisa mama na yule unayejifunza kwake (kiongozi wako). Unaweba kumuomba mchungaji ahubiri mtiririko wa jumbe kutoka katika kazi tano muhimu za kanisa kuandaa kusanyiko kuelewa na kuishika kazi yake.

Utakapowasilisha kauli ya maono na kauli ya dhima, waulize washirika ikiwa wamekubaliana nazo na kuwa tayari kuziunga mkono. Wakaribishe washirika wajitoe kufanya kazi ya kuzitekeleza kwa pamoja.

Ikiwa timu ya kuzindua na kanisa mama hawakukubaliana na maono na dhima kama ilivyoelezewa na viongozi, itakuwa ngumu sana kufanya huduma na mabadiliko muhimu ili kufikia maono kupitia utendaji kazi. Mpanda kanisa, viongozi wa kusanyiko, timu ya kuzindua lazima wawajibike ili kufikia makubaliano ya maono na utendaji kazi kabla ya kufanya kazi mabadiliko ya muhimu yoyote.

## **KIPINDI CHA 5**

# **MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MAADILI (Dakika 60)**

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Tumia masomo hapo chini kutoa utangulizi wa mawazo ya Kauli ya Maadili ya Msingi. Ongoza kundi kumaliza shughuli inayofuata.

### **NAMNA YA KUTENGENEZA KAULI YA MSINGI YA MAADILI (dakika 15)**

Rudia & Wazo Jipyta

#### **Rudia**

MAONO yanaelezea Mungu anavyotaka UWE.

DHIMA inaelezea kile Mungu anachotaka UFANYE.

#### **Dhana Mpya**

MAADILI YA MSINGI yanaelezea NAMNA UTAKAVYOENENDA unapotekeleza DHIMA ili kufikia MAONO.

### **MIFANO MIWILI YA KAULI YA MAADILI YA MSINGI:**

#### **1. Maadili ya Msingi ya Kanisa la Rock of Salvation (yalivyoelezewa kwa vitendo)**

##### **Kama watu wa Mungu, tumejitoa:**

- Kufanana na taswira ya Kristo kwa mtu binafsi na kwa kundi (Warumi 8:29; 2Wakorintho 3:18).
- Kuisema kweli kwa upendo (Waefeso 4:15, 25, 29), katika kusahihisha na kuonya, na kwa uwazi kwa kuzingatia maamuzi na masuala ya kiuchumi.
- Kila mmoja kumhudumia mwenzie kwa upendo, kutambua karama ya kila mmoja na kumpatia nafasi ya kuitumia (Warumi 12:1-8; 1Petro 4:10-11) na kuwafuasa watu wa rika zote na vipawa vyote (Kumbukumbu 6:20 & 11:18-21; Mathayo 28:18-20).

**Maadili ya Msingi ya Kanisa la Living Water (elezea vitu na vitendo kwa maneno)**  
**Kama jamii ya Wakristo, tunathamini:**

- Uwazi na umuhimu wa kuhubiri neno la Mungu (Mathayo 28: 18-20; 2Timotheo 4:2)
- Kuabudu kulenge Utatu Mtakatifu wa Mungu na siyo vipaumbele vyetu/ matamanio yetu. (Kumbukumbu 5:6-10)
- Huduma kwa wahitaji ndani na nje ya kusanyiko (Marko 12:31; Waefeso 5:1-2)
- Uanafunzi uwe kwa watu kuanzia watoto hadi watu wazima (Mathayo 28:18-20; Kumbukumbu 6:20 & 11:18-21)
- Kuwafahamu na kuwahudumia ndugu zetu katika Kristo waume na wake (Waefeso 4:2,25-32)
- Viongozi watumishi na washirika watakaotumia karama zao (Mathayo 20:25-28; 1Petro 4:10-11)
- Kuwajibika katika uwakili wa rasilimali (Zaburi 24:1)

Kawaida Kauli ya Maadili ya Msingi ni pamoja na maadili 3-7. Kauli ya maadili iwe fupi iweze kukumbukwa kwa urahisi.

Mara nyingi shughuli zilizotajwa katika kauli ya maadili ya msingi zimetajwa kwenye kauli ya dhima. Tofauti ni kwamba katika kauli ya maadili ya msingi, shughuli hizi huonyeshwa kama matokeo ya tabia fulani mahsus. Kwa mfano, maadili ya msingi ya Kanisa la Living Water yanetaja sio tu “kuabudu” bali aina ya kuabudu iliyo muhimu: kuabudu kumlenge Mungu na siyo matamanio ya mwanadamu, ambayo inaonyesha tabia ya haki. Maadili ya msingi yanatumika kama matarajio ya msingi ya kusanyiko kwamba viongozi wataliongelea/kutolea taarifa wakati wa kufanya maamuzi, kutathmini viongozi, kuwahudumia washirika n.k.

Maadili yote ya msingi sharti yawe na msingi wa Kibiblia. Maadili lazima yaungwe mkono na vifungu vya maandiko au kanuni iliyofundishwa katika maandiko.

Tunashauri kwamba maadili yako yapange kwa mtiririko wa vipaumbele. Mara nyingi kuongoza ipasavyo kunahitaji mtu au kusanyiko kupambanua kati ya maadili yenye kipaumbele. Kuweka maadili katika mtiririko wa kipaumbele itasaidia kuongoza aina hizi za maamuzi. Kwa mfano, ikiwa maamuzi au shughuli zinazounga mkono maadili #5 zinahitaji kukubaliana na maadili #1, basi maadili yaliyowekewa kipaumbele yataonyesha kwamba maamuzi na shughuli zinazounga mkono maadili #5 zirudiwe kufanyiwa kazi tena (au kwa namna nyingine ziachwe) ili kwamba kusanyiko libaki katika kweli ya maadili ya

muhimu zaidi.

## MPANGO KAZI WA SOMO LA 4

Kutengeneza Maadili ya Kanisa Jipya Lililopandwa (dakika 15)

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Soma maelekezo ya kazi na ujibu swalì lolote kutoka kwa washiriki.

1. Shughulika pamoja na mchungaji wako, viongozi kutoka kanisa linalokuunga mkono, na washirika wa kanisa jipya lililopandwa (kama tayari una washirika) kuendeleza kauli ya maadili ya msingi. Tunashauri kundi liwe la watu 5 hadi 9. Gawanya washiriki katika makundi ya watu watatu au wane. Katika kila kundi:
  - Soma MAONO na DHIMA yako tena.
  - Soma mifano miwili ya maadili ya msingi. Yanaweza kukupa mwongozo utakapokuwa unafikiria maadili ya msingi ya kusanyiko lako.
  - Bainisha maadili ya muhimu yanayoungwa mkono kibiblia yatakayoakisi mnavyotaka kufanya kama kusanyiko. (Katika muktadha wa kiutamaduni wa kanisa lako, maadili mengine zaidi ya yale yaliyotolewa kama mfano hapo juu yatapaswa kukaziwa.)
  - Chagua maadili 5-7 ya muhimu yatakayozungumzia namna kusanyiko lako na viongozi wake watakavyofanya katika miaka ijayo. Kuna maadili mengi yanayoweza kutambuliwa – unatakiwa uchague lile moja la muhimu kabisa kwa ajili ya kusanyiko lako sasa hivi, yale yatakayoongoza na kubeba MAONO na DHIMA yako.
2. Waambie kila kundi lisome orodha ya maadili yao ya msingi. Angalia msingi wa kibiblia kwa kila maadili.
3. Kwa pamoja angalia maadili ya msingi 5-7 ambayo yanazungumzia jinsi Mungu anavyotaka kusanyiko lenu lifanye katika miaka mitatu hadi mitano ijayo.
4. Soma orodha ya maadili ya msingi mbele ya kusanyiko lako ikiwa ni pamoja na misingi ya kibiblia, ikielezea kwa nini umechagua kila maadili. Waambie washirika washauri na kutoa mawazo. Rekebisha orodha ya **maadili kama ni muhimu, lakini hakikisha maadili ya msingi yanasisimamia katika Neno la Mungu.**

5. **Toa nafasi (kwa mfano, huduma maalum ya kujitolea) kwa washirika wote wa kanisa kujitolea wenyewe kuishi kulingana na haya maadili ya msingi.**
6. **Ujiandae kushirikisha kauli yako ya maadili ya msingi wakati wa Somo la 4. Jiandae kujadili mchakato ambao umeuhusisha kuendeleza Kauli ya Maadili ya Msingi.**

**Andika Kauli yako ya Maadili ya Msingi hapa:**

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

**Mapumziko (dakika 15)**

## KIPINDI CHA 6

# MPANGO WANGU MKUU WA KUPANDA KANISA: MKAKATI (Dakika 60)

### MAREJE & DHANA MPYA (DAKICA 15)

#### Marejeo

MAONO yanaelezea Mungu anavyotaka UWE.

DHIMA inaelezea kile Mungu anachotaka UFANYE.

MAADILI YA MSINGI yanaelezea namna Mungu anavyotaka UENENDE.

#### Wazo Jipy

MKAKATI ni mkusanyiko wa vitendo mahususi ambavyo utavitimiza ili kukamilisha MAONO na DHIMA yako wakati ukiyaishi MAADILI YAKO MSINGI.

**Sema**, “Katika Somo la 1 ulipewa utangulizi wa Hatua Tano za Kupanda Kanisa na Mzunguko wa Kupanda Kanisa”.

Waongoze warudie kuanzia Somo la 1 mafunzo ya Hatua Tano za Kupanda Kanisa na Mzunguko wa Kupanda Kanisa.

**Sema**, “Muhtasari ufuatao umejumuisha mawazo haya mawili kutoa mpango wa mkakati wa kupanda kanisa. Kazi yako ni kutafuta na kuandika matendo pekee 3 hadi 5 ambayo utayachukua kwa kila sehemu ya mkakati. Kama angalizo kwa Maono na dhima yako, mkakati wako uakisi kile ulichojifunza katika utafiti wako.”

**MAENDELEO YA MKAKATI WA KUPANDA KANISA**  
**MKAKATI WANGU WA KUPANDA KANISA**

A. Maombi

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

B. Uinjilisti

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

C. Uanafunzi

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

D. Ushirika (Kukusanyika Pamoja)

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

E. Kukuza Uongozi

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_

5. \_\_\_\_\_

F. Kuabudu

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

G. Huduma

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

H. Kujizidisha (Dhima)

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

## MPANGO KAZI WA SOMO LA 4

Boresha Mkakati wako wa Kupanda Kanisa

Utakapopitia na kuendeleza Kauli yako ya Maono, Kauli ya Dhima, na Kauli ya Maadili ya Msingi pamoja na mchungaji wako na kundi la kuzindua, pia shirikisha na rekebisha mkakati wako katika mchakato huu.

## KUFUNGA

Ni nini kinachofuata?

- Rudia Mipango Kazi mitatu katika Somo la 4 (angalia sehemu ya 7,8 na 9 katika muongozo huu). Jibu swali lolote linalofanana nayo.
- Waambie wajitolee kushirikisha majibu ya maswali yafuatayo kwa maneno yao wenyewe:
  1. Kauli ya Maono ni nini? (angalia kipindi cha 3)
  2. Kauli ya Dhima ni nini? (angalia kipindi cha 4)
  3. Kauli ya Maadili ya Msingi ni nini? (angalia kipindi cha 5)
  4. Mkakati wa Kupanda Kanisa ni nini (angalia kipindi cha 6)
- Waambie washiriki washirikishe jambo jipya walilojifunza katika mafunzo ambalo linaleta mwamko, linatia moyo, au linalowapa motisha kama wapanda makanisa.
- Mwambie kila mshiriki aamue malengo yake ya Kupanda Kanisa kwa mwezi huu.
- Imbeni wimbo wa kuabudu pamoja na mfunge kwa maombi ya baraka kwa ajili ya hawa wapanda makanisa.

**Angalizo kwa Mwezeshaji:** Kama una muda wa ziada kwa sababu kipindi cha 5 cha mafunzo haya hakitachukua dakika 60 zote, unaweza kutumia muda wowote wa ziada kwa kadiri ya uhitaji, kwa mfano, kwa kupitia masomo yaliyotangulia, mafundisho, maombi katika vikundi vidogo, kushughulikia maswali na changamoto walizo nazo washiriki, au kuwatawanya mapema.

Mpango Kazi wa Somo la #4: kupitia orodha

- Boresha na shirikisha kauli za maono na dhima (angalia Kipindi cha 3 na cha 4)
- Boresha na shirikisha kauli ya maadili (angalia Kipindi cha 5)
- Shirikisha na pitia mkakati wako wa kupanda kanisa (angalia Kipindi cha 6)
- Fanyia kazi malengo yako ya kupanda kanisa kwa mwezi huu (angalia Kufunga)

<b>MALENGO YA KUPANDA KANISA KWA MWEZI HUU</b>	
<b>WATU BINAFSI</b>	
Watu wapya uliowafikia	
Waongofu wapya	
Watu Wapya Waliobatizwa	
Viongozi wapya katika mafunzo	
<b>MAKUNDI MADOGO</b>	
Makundi madogo mapya	
Washiriki wapya katika makundi madogo	
Viongozi wapya na makundi madogo	